

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA



CHUO CHA MAAFISA TABIBU KILOSA

**TANGAZO KWA WANAFUNZI WALIOHITIMU MAFUNZO YA UTABIBU KABLA YA
MWAKA 2020 KATIKA CHUO CHA MAAFISA TABIBU KILOSA AMBAO
HAWAJACHUKUA VYETI VYAO VYA TAALUMA**

Mnamo tarehe 15 Aprili 2019 chuo cha Maafisa Tabibu Kilosa kilipata janga la moto lililotekeza baadhi ya majengo ya chuo ikiwemo jengo la ofisi za utawala wa chuo. Katika janga hilo mali mbalimbali zilizokuwemo katika majengo hayo ikiwemo vyeti vya kitaaluma vya wahitimu ambao walikuwa bado hawajavichukua. Vyeti vilivyoathirika ni vya wahitimu wa miaka ya nyuma ya 2019.

Kufuatia changamoto hiyo, Chuo kimeshachukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwasiliana na mamlaka ya utunuku wa vyeti hivyo (NACTVET na Wizara ya Afya) ili kuwezesha wahitimu wao kuandaliwa vyeti vyao upya. Ili kuhakikisha wahitimu wote ambao hawakuchukua vyeti vyao wanaandaliwa vyeti hivyo, Mkuu wa Chuo anawatangazia wahitimu hao kuwasilisha barua za maombi ya vyeti vya kuanzaia tarehe 17 Aprili, 2023 hadi 31 Mei, 2023. Barua hizo zitumwe kupitia barua pepe principal.kilosacote.go.tz au kwa njia ya posta kwa anuani ya Mkuu wa Chuo, Chuo cha Maafisa Tabibu Kilosa, SLP 150, Kilosa. Baada ya kupokea barua hizo Chuo kitafanya uhakiki wa taarifa kabla ya kuwasilisha kwa mamlaka husika na zoezi hilo litakuwa limefungwa rasmi.

Chuo kinawaomba radhi kwa usumbufu wowote ulikwishajitokeza kufuatia changamoto hiyo. Atakayesikia tangazo hili amtaarifu na mwenzake.

Imetolewa na:

Dkt. Sospeter Benjamin Mangwella

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Sospeter Benjamin Mangwella'.

Mkuu wa Chuo, Chuo cha Maafisa Tabibu-Kilosa

17 Aprili, 2023